**BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

# HOTUBA YA KAMATI YA BAJETI YA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU MSWADA WA SHERIA YA KUTOZA KODI NA KUFUTA BAADHI YA KODI NA TOZO NA KUREKEBISHA BAADHI YA SHERIA ZA FEDHA NA KODI ZINAZOHUSIANA NA UKUSANYAJI NA UDHIBITI WA MAPATO YA SERIKALI NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

## UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** Awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu (S.W) kwa kunijaalia afya njema na uzima nikaweza siku hii ya leo kusimama mbele ya Baraza lako kwa ajili ya kutoa maoni ya Kamati kuhusiana na Mswada wa Sheria ya Kutoza Kodi na Kufuta baadhi ya Tozo na Kodi na Kurekebisha Baadhi ya Sheria za Fedha na Kodi Zinazohusiana na Ukusanyaji na Udhibiti wa Mapato ya Serikali na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo kwa Mwaka Fedha 2022/2023.

**Mheshimiwa Spika,** Napenda kukushukuru wewe kwa dhati kabisa kwa kunipa nafasi hii kutoa maoni ya Kamati ya Bajeti kuhusiana na Mswada huu. Aidha, nawashukuru na kuwapongeza Wajumbe wa Kamati yangu kwa namna wanavyonipa ushirikiano mkubwa katika kuiongoza Kamati hii. Maoni na ushauri wao wanaonipatia kwa kiasi kikubwa unasaidia katika kutekeleza majukumu ya mbali mbali kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** Hotuba hii ni matokeo ya michango ya wadau mbali mbali ikiwemo wanasheria kutoka Afisi ya Baraza la Wawakilishi ambao waliisaidia Kamati katika kutupatia ufafanuzi wa vifungu vya mswada.

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya utangulizi huo, naomba uniruhusu niwatambue Wajumbe wa Kamati kama ifutavyo:

| | |
|---|---|
| 1. Mhe. Abdalla Hussein Kombo | Mwenyekiti |
| 2. Mhe. Asha Abdalla Mussa | Makamo Mwenyekiti |
| 3. Mhe. Fatma Ramadhan Mohammed | Mjumbe |
| 4. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu) | Mjumbe |
| 5. Mhe. Miraji Khamis Mussa | Mjumbe |
| 6. Mhe. Prof. Omar Fakih Hamad | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Sekretarieti, Kamati yetu ina makatibu wanne, naomba nichukue fursa hii kuwashukuru kwa ushauri wao katika kufanikisha majukumu yetu na naomba kuwatambua kama ifuatavyo:

| | |
|---|---|
| 1. Ndg. Abass Vuai Moh’d | Katibu |
| 2. Ndg. Asha Said Mohamed | Katibu |
| 3. Ndg. Husna Rajab Othman | Katibu |
| 4. Ndg. Shaib Fadhil Shaib | Katibu |

## UCHAMBUZI WA MSWADA

**Mheshimiwa Spika,** Madhumuni ya Mswada huu ni kurekebisha Sheria mbali mbali za Fedha na Kodi zinazohusiana na ukusanyaji na usimamzi wa Mapato ya Serikali na Mambo mengine yanayohusiana na hayo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yangu iliupitia Mswada huu na kuibua marekebisho mbali mbali, baadhi ya marekebisho hayo ni pamoja na marekebisho ya kisarufi ambapo vifungu mbali mbali vimerekebishwa ili kuvifanya visomeke vizuri na vilete maana iliyokusudiwa, marekebisho mengine yaliyopendekezwa na Kamati yangu ni kufanya marekebisho yanayotokana na makosa ya kiuchapaji kwa lengo la kuweka bayana usahihi wa maneno hayo.

**Mheshimiwa Spika,** Miongoni mwa Sheria zinazorekebishwa ni Sheria ya Utaratibu na Usimamizi wa Kodi, Nam. 7 ya mwaka 2009 ambapo kumeongezwa kifungu kipya cha 53C mara baada ya kifungu cha 53B. Kamati inaunga mkono marekebisho haya pamoja na kusisitiza marekebisho haya yazingatie makubaliano ya bei ya kabla ya kulipa kodi kama yalivyoainishwa katika kifungu hichi. **Mheshimiwa Spika,** ifahamike kuwa, makubaliano ya bei ya kabla ya kulipa kodi ni kwa muda maalumu na iwapo mlipa kodi atashindwa kufuata masharti yaliyowekwa, anaweza kufutiwa kodi hiyo baada ya Kamishna kupata idhini ya kuifuta kutoka kwa Mheshimiwa Waziri. Hivyo, ni muhimu kwa mlipa kodi kuzingatia masharti aliyoingia katika makubaliano hayo.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa vile marekebisho ya Sheria ya Utaratibu na Usimamizi wa Kodi, Nam. 7 ya mwaka 2009 yanakusudiwa kuondosha ukwepaji wa kodi kwa baadhi ya wafanyabiashara wa hoteli pale wanapoondoka nchini bila ya kulipa madeni ya kodi. Ili marekebisho haya yalete ufanisi kwa haraka na kuweza kuzuia mianya ya upotevu wa mapato, Kamati inaishauri Serikali kwa kutumia Sheria hii sasa, itunge kanuni zitakazotoa miongozo ya uwekaji dhamana katika uendeshaji wa biashara hiyo haraka iwezekanavyo.

**Mheshimiwa Spika,** Katika marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma Nam. 12 ya 2016 pamoja na mambo mengine, Serikali inakusudia kutayarisha kanuni za miongozo ya utoaji wa misamaha ya kodi ili kusimamia, kudhibiti pamoja na kuongeza ufanisi katika utoaji wa misamaha hiyo. Kamati inapata faraja sana kwa hatua hii kwa sababu misamaha ya kodi imetumika vibaya kwa muda mrefu. Lengo la misamaha ya kodi ni kuwavutia wawekezaji na kutoa unafuu kwa taasisi ambazo zinalenga kutoa huduma kwa jamii moja kwa moja. Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha kuwa kanuni hizo zinatungwa na kutekelezwa kwa haraka. Jambo hili ni jema kwani litaleta nidhamu katika mapato na kuongeza makusanyo yetu.

**Mheshimiwa Spika,** Sheria nyengine inayorekebishwa katika Mswada huu ni Sheria ya Mamlaka ya Kukuza na Kulinda Uwekezaji Zanzibar, Nam. 14 ya mwaka 2018 ambapo Serikali inakusudia kutayarisha muongozo kwa Mawaziri wasiyohusika na mambo ya fedha kuingia mikataba na wawekezaji yenye vipengele vya kikodi bila ya kushauriana na Waziri anayehusika na mambo ya fedha. Kamati inaunga mkono marekebisho haya kwani yataleta nidhamu katika masuala yanayohusu kodi pamoja na kuweka utaratibu mzuri kwa Mawaziri kutekeleza majukumu ya sekta wanazozisimamia bila ya kufanya mamuzi kwa mambo yanayohusiana na kodi isipokuwa baada ya kushauriana na Waziri anayehusika na mambo ya fedha.

**Mheshimiwa Spika,** Marekebisho ya Sheria ya Mamlaka ya Kukuza na Kulinda Uwekezaji Zanzibar, Nam. 14 ya mwaka 2018 vile vile yanakusudiwa kudhibiti wawekezaji ambao wanaitumia vibaya misamaha ya kodi. Kamati inaipongeza sana Serikali kwa uamuzi huu ambao unatarajiwa kuondosha uvujaji wa mapato kwa kutumia vibaya

misamaha ya kodi inayotolewa. Hivyo, Kamati inaisisitiza Serikali kusimamia vyema jambo hili ili kuhakikisha marekebisho haya yanatekelezwa kwa vitendo na hatimae kuinufaisha nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,** Sheria nyengine inayorekebishwa katika Mswada huu ni Sheria ya Ongezeko la Thamani Nam. 4 ya 1998 ambapo Serikali inakusudia kuimarisha huduma za utoaji wa mikopo kwa Benki za Kiislamu kwa kuondoa changamoto  za utozaji wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) mara mbili ambapo kodi hutozwa wakati Benki inaponunua bidhaa na wakati wa kuwasilisha bidhaa hiyo kwa wateja. Kamati inaafikiana na marekebisho haya kwani yataleta unafuu kwa wananchi pamoja na kuimarisha sekta ya fedha katika nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande mwengine, marekebisho ya Sheria ya Ongezeko la Thamani Nam. 4 ya 1998 yanalenga kuanza kutoza kodi kwenye huduma zitolewazo mitandaoni. Jambo hili litasaidia sana kuimarisha makusanyo ya mapato yetu. Kamati inaafiki hatua hii na inaiunga mkono. Aidha, Kamati inasisitiza katika utekelezaji wa marekebisho haya, Serikali ihakikishe inawashirikisha kwa kiasi kikubwa wadau wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kwani jambo hili linahusu mambo ya kitaalamu sana katika TEHAMA.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kumalizia, ili lengo la kupata ufafanuzi wa kina wa baadhi ya marekebisho yaliyopendekezwa na Kamati ya Bajeti, nawaomba Wajumbe wako waupitie waraka wa Kamati wa Mapendekezo ya Marekebisho ya Mswada huu ambao wamepatiwa.

**Mheshimiwa Spika,** Mwisho kabisa, Kamati ya Bajeti inasisitiza kwa mara nyengine juu ya uwasilishwaji wa nyaraka zote zinazopitia katika ngazi ya Kamati kabla ya kuletwa katika Baraza, ziwasilishwe mapema ili

Wajumbe wapate fursa pana ya kuzijadili, kutoa maoni yao na hatimaye kuweza kuishauri Serikali ipasavyo.

## HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** Naomba nihitimishe kwa kuwashukuru Wajumbe wa Baraza lako kwa kunisikiliza kipindi chote nilichokuwa nawasilisha maoni ya Kamati yangu. Aidha, nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii.

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya shukrani hizo, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wauchangie, waujadili na kuupitisha Mswada huu kwa lengo la kurahisisha utekelezaji wake pamoja na kuzipa fursa taasisi zilizopewa majukumu ya kukusanya mapato kuweza kutekeleza majukumu yao.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba kuwasilisha

Ahsante.

Mhe. Abdalla Hussein Kombo,
Mwenyekiti,
Kamati ya Bajeti,
Baraza la Wawakilishi,
**Zanzibar.**